



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY – FOURTH SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 27th May 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 11:00 a.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

STATEMENTS

**RENOVATION OF THE SOCIAL HALL, TOILETS AND STAFF
QUARTERS AT ATC IN MTWAPA**

Hon. Ndago: Thank you Mr. Speaker. I would like to read a Statement through the Chairperson; Agriculture, Livestock and Fisheries Committee:-

Whether the CECM (County Executive Committee Member) in charge of the Department of Agriculture, Livestock and Fisheries is aware that the renovation of the social hall, toilets and staff quarters in ATC (Agricultural Training College) in Mtwapa are yet to be completed?

Whether the projects were tendered and if yes, what is the name of the contractor who won the tender and how much is paid so far in renovation to the projects? If yes, what measures is the CECM taking to ensure the projects are completed and handed over to the institute for immediate use? Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Next.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ABANDONED ENVIRONMENTAL PROJECTS IN MTWAPA

Hon. Ndago: Thank you. I would also like to read a Statement through the Chairperson; Water, Environment and Natural Resources Committee:-

Whether the CECM in charge of the Department of Water, Environment, Natural Resources and Solid Waste Management is aware that the above projects which entailed the planting of flowers had started but maintenance of the same was abandoned.

What is the name of the contractor awarded the contract and whether the contract agreement did not include the maintenance of the said flowers? How much has been paid so far to the contractor? If yes, what measures is the CECM taking to ensure the projects are properly maintained to ensure the dignity of Mtwapa town is sorted as per the initial plan? Thank you.

MOTION

APPROVAL OF REVIEWED LIST OF COMMITTEES MEMBERSHIP

THAT, Pursuant to the provisions of Standing Order Nos. 163 and 165, this honourable Assembly approves the attached list of reviewed Committee membership to the Select Committees on Implementation and Delegated County Legislation; and the Sectoral Committees by the Select Committee on Selection.

(Hon. Chiriba on 20.5.2020)

(Resumption of Debate interrupted on 20.5.2020)

The Speaker (Hon. Kahindi): The Motion was for the approval of new list of committee Members to the Select Committee on Implementation and Delegated County Legislation and the Sectoral Committees. The reason for the deferment of that Motion was that it had not complied with the provisions of the Standing Orders in the sense that the Report was not laid in the House.

I am reliably informed that the Report has now been tabled and each Member has been able to receive a copy and we will resume the debate. I am also informed that hon. Chiriba was on the Floor before the debate was suspended. Hon. Chiriba, I give you priority you proceed from where you stopped.

Hon. Chiriba: Thank you Mr. Speaker. Yes I was on the Floor and I can remember that I had started by applauding the Committee for the work they did and especially by giving an opportunity to hon. Kiraga to join the Committee on Education.

As I stand today Mr. Speaker, I have also learnt the importance of the Assembly being served with the copy of the Report even before a debate is brought to the House. So having gone through the rest of the Committees, I have found that the Membership of the Committees is intact and as I know, we have an awaiting by-election in Dabaso Ward so I am starting to wonder where or how or when that Member comes to this hon. House which Committee will this hon. Member serve? I am seeing some weakness in the same and I withdraw my sentiments on support to the Motion and thus disapprove this Report. I stand to oppose. Thank you.

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker, for giving me this chance to contribute to this very important Motion. I stand to oppose this Report. If you look at the composition of the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Committees and I want to be very specific on the Committee on Water, Environment and Natural Resources that is Committee number two; the composition and the names here are 13, and in Kilifi County we have seven Sub-Counties. I expected to at least have a Member in every Sub-County for representation purposes. For instance, Magarini is not represented here. It is very important that at least in every Committee since we have a composition of 13 Members we get at least one Member from every Sub-County so that we can have all of them fully represented.

(Hon. Mwarandu stood on Point of Order)

Hon. Mwarandu: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. It is not a Point of Order as such; it is a Point of Information to hon. Peter Ziro.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Ziro do you wish to be informed?

Hon. Ziro: No Mr. Speaker.

Hon. Mwarandu: I will proceed to a Point of Order No. 161 Sub-Order (1) (a);

“The membership of each committee reflects the reflective majority of the seats held by each of the Assembly parties or coalition of the parties in the County Assembly”.

Mr. Speaker, when it comes to composition of membership in Committees, we are not here to say we should select Members from these Sub-Counties. It is purely on strength of parties. So coming here saying a Member should come from Magarini or Rabai is...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Peter Ziro is only trying to give his reasons why he doesn't support the Report ...

(Loud consultations)

You can say maybe he is misleading the House but you cannot say his debate is improper. He is only trying to convince you; it is up to you to decide. However your Point of Order is noted.

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, for informing him. The Committee on Selection is guided by the provisions of the law however; the Member is entitled to make his contribution whichever way he feels like.

Mr. Speaker, why I am saying this is because water is a very important commodity. It is required everywhere. Water is life! More than 70 percent of the body composition of a human being is water. Therefore, Magarini Sub-County Membership in this Committee is lacking. So I stand to oppose this Report. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Water is important but the law is also provided for.

Hon. (Ms.) Maneno: Thank you Mr. Speaker, Sir for this chance. I stand to support the Motion of approval of the reviewed list of Committees. The Committee did a very good job; they considered Standing Order No. 152 (b), the parliamentary parties and also considered the independent party Members. Therefore I support the Report. Thank you.

Hon. Kadenge: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Naungana na waheshimiwa wenzangu wa Jilore na Garashi kupinga mjadala huu. Nikiangalia hivi katika Idara ya *Trade, Tourism and Cooperatives* naona kuna mheshimiwa Christopher Mwambire. Huyu amebobea sana katika sheria ya administration maanake amekuwa naibu wa chifu. Sasa ukimueka katika Idara ya *Trade and Tourism* hapa tutakuwa tumekosea na tukienda pia kwa Idara ya Afya kuna mheshimiwa jirani yangu Edward Kazungu Dele...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Laughter)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kadenge, I know you are entitled to your argument but are you implying that a Member of this House is incompetent to serve in the Committee? The criteria for Membership into Committees are clearly stipulated. Why I am saying so is that it is not fair to argue that a Member has been a Sub-Chief because there is no criteria for joining the County Assembly. I do not want it to go on record that the hon. Member was belittled and especially when he is not present.

As Members of the County Assembly, there is no minimum academic requirement so you cannot say because he was a Sub-Chief. You can make your argument without mentioning names.

Hon. Kadenge: *Point* yangu ilikuwa ...

The Speaker (Hon. Kahindi): Kindly make your point clear so that we understand you. Were you implying that he is incompetent?

Hon. Kadenge: No!

The Speaker (Hon. Kahindi): Then proceed.

Hon. Kadenge: Nilikuwa napeana mfano ya kuwa kila Kamati iwekwe watu ambao wameisomea. Kwa mfano, kama mheshimiwa Kadenge ni *retired tourism officer* na nafikiri akiwekwa hapa itakuwa si vibaya kwa sababu miaka yote ambayo nimekuwa kwa *hotel industry* nimekuwa kwa hii *tourism*. Lakini kumueka naibu wa chifu nafiki tumtafutie mahali pake...

(Hon. Kenga stood on a Point of Information)

Hon. Kenga: Mr. Speaker, it is a point of information to the Member, he is my Chair Devolution ...

Hon. Kadenge: No! I don't want to be informed.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kadenge, do you wish to be informed?

Hon. Kadenge: Okay because he is my Deputy Speaker, you can inform me.

Hon. Kenga: Mr. Speaker, I just wanted to inform my Chair Devolution that for this Assembly to have a Member who was initially a Sub-Chief, to me this is a great honour and an achievement. So let us not waste it; I mean the wealth of experience that he has garnered in the field of administration as a Sub-Chief can be applied in most of the Committees.

I know the kind of work Sub-Chiefs are dealing with on the ground. Therefore, I want to believe that he is in a position to serve in any Committee in this Assembly for having been a Sub-Chief.

Hon. Mwathethe: Kwa sababu mheshimiwa Kadenge Dadu alikuwa akiongea Kiswahili, wacha na mimi nijaribu kuongea Kiswahili. Bw. Spika, ni jukumu lako kuelekeza changizo katika hili Bunge na kama ulivyokuwa ushasema tayari kwamba uchaguzi wa Kamati haulinganishwi na elimu ambayo mtu yuko nayo bali akiwa yeye ni mheshimiwa anaweza kuingia katika Kamati yoyote.

Hata hivyo, nataka nimueleze mheshimiwa Kadenge kwamba tuko na Kamati ya *Justice and Legal Affairs*; labda hii ingetaka wasomi ambao wamesomea sheria. Atuambie ni kina nani na nani hapa ambao wangeingia pale kwa sababu wako na elimu hiyo ndio sasa tutakaporudi tujue tunatakiwa kuweka hapo nani na nani. Nitasisitiza kwamba si lazima uwe umesomea kitu ndio uweze kwenda pale. Ikiwa ni hivyo, basi hata kwa Kamati ya *Health* hatutaweza kuweka

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

madaktari maana hatunao isipokuwa mheshimiwa Kiraga tu. Ikiwa huo ndio muelekeo, basi itakuwa mheshimiwa Kadenge anatudanganya na anatuongoza katika barabara ambayo siyo. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Members, before you make any contribution you need to be aware of Standing Order No. 161. It is purely a political party issue and you don't need credentials. That is why I sometimes say if things were taken literally then we would also not fit anywhere. When we talk of the Justice and Legal Affairs Committee, it is only in the Senate where the bigger percentages are lawyers.

I want to take that hon. Kadenge was saying that on a light note and to also concur with the Deputy Speaker on what he has said. Chiefs are administrators. If we go by our academic qualifications then some of the Committees will be left un-attended to. We just have to be Members then learn in those Committees. So our arguments should not strictly be on academics because when we talk about academics, there was no degree required for you to be a Member of the County Assembly. It is just secondary education. So I want to take it that and the reason that hon. Member for Bamba is silent but you know the implication that that has on the record is something and that is why I have taken it up to guide you so that we argue it on the right path. Conclude hon. Kadenge.

Hon. Kadenge: Waheshimiwa wenzangu, *point* yangu ni kuwa kama Chair mnafanya huu uchaguzi wa Kamati, najua si rahisi kupata watu kulingana na kiwango cha elimu lakini tuanze pia kuangalia kila mmoja pale ambapo anastahili tukikosa kabisa ndio tunaenda huko kwengine; *that was my point of argument*.

The Speaker (Hon. Kahindi): No...no...no... You are mixing your language hon. Dadu (Kadenge).

Hon. Kadenge: Kwa hivyo, mimi nikiangalia hii orodha ambayo iko katika hii *list* ninapinga na ninaomba ile *Committee ya Selection* ikakae na izingatie vile ambavyo ninasema mimi. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Saumu (Sidi)

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you Mr. Speaker for this opportunity to also air my sentiments. First, I start by applauding the Committee on Implementation and Delegated Legislation under the Leadership of our very able Majority Leader for having seen it wise first to adhere to Standing Order No. 231. Mr. Speaker, this is one of the Committees which I would say in this whole Assembly has set a very good precedence ...

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Stanely, you have a Point of Order?

Hon. Kenga: Mr. Speaker, the Leader of Majority has been referred to as a Chairperson of a Committee that I do not think he chairs. I do not think he is a Chairperson of the Implementation and Delegated Legislation.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, I have also noted that...

(The hon. Speaker spoke off record)

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you also my very able Deputy Speaker for that correction. I wish to proceed. As I was saying Mr. Speaker, this is one of the Committees that have set a very good precedence for this Assembly.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, you understand that Standing Order No.231 allows this Committee to do reviews and we have seen that in their wisdom they have seen it very wise to increase the number of membership from the previous of nine to thirteen. This is a good precedence not only for us but even for the people to come because now we will see committee membership will be made of thirteen people and that is a very good thing to congratulate the committee for. Also if you check at the committee findings Mr. Speaker, you will ...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Saumu (Sidi), you need to quote the right Standing Orders with what you say. Standing Order No. 231 is the review of...

(The hon. Speaker spoke off record)

...that will be the Committee on Procedure and Rules and not the Committee on Selection.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you for that clarification. So, I was saying if you also check at their findings you will see that Committee finding number one says that they have retained the membership and only added four for the purposes of meeting especially Standing Order No. 161 (2) and some of the Sub-Orders one and two but specifically I am touching on Standing Order No. 161 (2). If you go into each and every Committee, you will see that the point of 2/3 gender rule has really been upheld and that is a good thing for the Committee. With those few remarks, I strongly support this Motion. Thank you.

Hon. Shaban: Asante mheshimiwa Spika. Mimi pia nimesimama kuunga mkono serikali ya mheshimiwa Gavana kupitia kwa *Leader of Majority*. Mheshimiwa Spika, huu ni Mswada wa Serikali na ni lazima tuunge mkono vilivyo na pia nataka pia tufahamu kwamba tuko na mheshimiwa mgeni mheshimiwa Christine John ambaye ni mjumbe maalum ambaye tokea aingie katika Bunge hili mheshimiwa Spika hana Kamati; sisi wajumbe wote tuko katika Kamati. Tunakuja Bunge na mbali na Bunge, tuko na vikao vyengine vya Kamati na mheshimiwa Spika unaelewa ukikaa katika kikao cha Kamati mambo ambayo yanajiri. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, mimi naona tusipopitisha Mswada huu tutakuwa yule mheshimiwa mjumbe maalum tunamtenga na tunafanya anakuwa yatima katika hili Bunge.

Wakati mwingine ananipigia simu namwambia mheshimiwa mimi niko katika Kamati nitakupigia baadaye na anasema mbona mimi sijakuwa katika Kamati. Kwa hivyo, mimi naona mheshimiwa Spika, hii ni fursa ya yeye pia awe katika Kamati ili aweze pia kuchangia katika Kamati yake ili aweze kuwakilisha vizuri watu wa ile sehemu ambayo amechaguliwa kuwakilisha Bunge hili. Kwa hivyo mheshimiwa Spika naungana na *Leader of Majority* kisha nimshukuru mzee wetu wa busara, hana maneno; anachapa kazi ndio maana hata akishindwa kesi kule wadi anarudishwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sitaki kuongea mengi lakini wakati wajumbe wanachangia Mswada huu tumuangalie mheshimiwa Christine John *a.k.a* Riziki kwamba amekuja Bunge na tokea aapishwe hajakuwa katika Kamati yoyote na naona mheshimiwa Spika Mswada huu ukianguka basi mheshimiwa Christine John atakaa muda mrefu sana kwa sababu nimesoma hizi *minutes* na nimeona kwamba kulikuwa na vikao vingi tangu waheshimiwa wawekwe katika hii *list*. Naona muda utakuwa unaenda na mheshimiwa tutakuwa tunamuacha gizani na atakuwa hana Kamati. Kwa hayo machache, asante mheshimiwa Spika.

Hon. Mwarandu: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ili pia nami niweze kuchangia mjadala ambao uko mbele yetu. Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwanza kabisa nauga mkono Mswada huu na nataka nishukuru Kamati hii kwa jumla na pia nataka nishukuru Kiongozi wa Walio Wengi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii na vile vile Kiongozi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wa Wachache Bungeni ambaye ni Naibu Mwenyekiti wa Kamati hii na wanakamati wote walioketi na kwa ushauri wao wakaona ni bora waelekeze wanakamati katika Kamati zile. Mheshimiwa Spika, viegezo ambavyo vyastahili tviangalie hapa ni, je sheria ililindwa kati ya ...

(Hon. Dele consulted loudly)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Dele, consult in a low tone. Yes proceed hon. Mwaranadu.

Hon. Mwarandu: Je, sheria ilifwatwa katika kugawanya wanakamati katika Kamati hizi? Na kwa mtazamo wangu mimi mheshimiwa Spika ni kwamba ndio, sheria ilifwatwa. Tukiangalia kwanza ile Kanuni ya Bunge, Kanuni ya 161 kwanza (a) na pia ile Kanuni ya pili ilifuatwa. Mheshimiwa Spika, haya mengine yote ni mambo ya chama na hivyo basi sitaki kusema kwamba nataka nimfundishe Kiranja wa Walio Wengi Bungeni kazi lakini nataka pengine awaite hawa wana ODM (*Orange Democratic Movement*) ili wachague wenyewe zile Kamati ambazo wao wenyewe wanataka kwa sababu kazi hii ni kazi ambayo imeelekezwa kwa Kamati ile ya uteuzi peke yake; hakuna yule mjumbe ambaye anastahili kujiweka mwenyewe katika Kamati. Ni Kamati hii ya uteuzi ambayo imepewa jukumu la kuteua wanakamati katika zile Kamati. Sasa tukija hapa tukianza kusema Kamati hii ilikuwa hivi Kamati ilikuwa hivi lakini kama ulivyoelekeza pale mwanzo mheshimiwa Spika, je sheria ilifuatwa? Je Kanuni za Bunge zilifuatwa? Hivyo vyote mheshimiwa Spika vilifuatwa. Asante mheshimiwa Spika.

Hon. Ndago: Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, nasimama kupinga Hoja hii kwa sababu ninavyoziangalia hizi Kamati zilivyo, naona nikitoneshwa vidonda. Mheshimiwa Spika, mimi nataka kukumbusha baadhi ya waheshimiwa waliozungumza ya kwamba ni ndani ya Bunge hili walileta Hoja tofauti, wengine wakaleta *statements* tofauti wakikosoa *department* hii na *department* ile.

Wengine ukiwaangalia bado wako katika zile *departments*. Kwa mfano, tukiangalia Wizara ya Afya, vile hali ya afya imekuwa katika Jimbo la Kilifi tukizugumza kando kando ya kwamba Kamati hazifanyi kazi na ukiangalia katika hiyo Kamati ya Afya, wale walioko hapo mimi ningeomba kupitia Bunge hili kufanywe marekebisho yarudishwe kwa Kamati. Nafikiri hata Kiongozi wa Walio wengi alipokuwa akizungumza tumemsikia kwa umakini waliosikiza semi za watu ya kwamba hata ikirudishwa nitaenda kurekebisha. Kwa hivyo, ana imani yeye mwenyewe ya kwamba haiko sawa. Nataka kuwaambia wale ambao wako upande wa Serikali, tuangalie vizuri tusipakwe mafuta kwa mgongo wa chupa...

(Hon. Mwathethe stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Mwathethe, you have a Point of Order?

Hon. Mwathethe: Mheshimiwa Spika, mimi sijasema ya kwamba Ripoti ikikataliwa nitaenda kurekebisha; mimi naamini Ripoti iko sawa ndio maana nimetia sahihi na kuileta mbele ya Bunge ikubali ama ikatae. Ikikataliwa itakuwa ni mambo ya kwamba imekataliwa lakini kwamba ina kasoro, nitaenda kurekebisha, mheshimiwa Spika hilo sijalisema na kama nimelisema lakini nimesehau basi nikumbushwe lakini sijasema hivyo.

The Speaker (Hon. Kahindi): The office of the Leader of Majority is really looking at...

(The hon. Speaker spoke off record)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Let us proceed. Hon. Ndago the Floor is yours...

Hon. (Ms.) Maneno: Mr. Speaker...

(Hon. (Ms.) Maneno stood in her place)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. (Ms.) Maneno, what is your Point of Order?

Hon. (Ms.) Maneno: Sijui kama utaniruhusu nimjuze mheshiwa Ndago. Kulingana na hizi ...

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, Hon. Ndago, do you wish to be informed?

Hon. Ndago: Singependa kujuzwa kwa sababu nimekaa kwa umakini na nikajua ni nini ninachokizungumza. Nilikuwa nasema kwamba tuwe na umakini wakati tunapitisha Hoja ama tunapopitisha maswala ya Bunge hili. Nataka tuangalie mkaazi wa Kilifi jinsi anavyoteseka upande wa afya. Wewe mwenyewe hapo ulipokaa kama mheshimiwa una ufahamu ni jinsi gani watu wanavyoteseka halafu tuangalie hii Kamati ya Afya vile imekuwa kwa kipindi hicho chote cha miaka mitatu; mtu wa Kilifi ameteseka na tena uangalie Kamati ya *Impementation*. Ni mambo mengi sana tumepitishwa hapa lakini havijawahi kufwatiliziwa na hizi Kamati ziko hapa. Na sisi tumekuwa tukisema tunaona watu wakifanya kazi. Wakati mwingine tunalia hapa ya kwamba kazi haifanyiki na wale wenye kufanya hizi kazi ni sisi wanakamati tuweke ile *Executive on toes*.

Hii Kamati mimi siiungi mkono ya kwamba warudi watu wale wale. Tukiangalia ile Kamati ya *Delegated*, angalau tuone Ripoti moja imekuja; moja tu kwa kipindi cha miaka miwili ama mitatu. Sasa hapa tunang'ang'ania tu tupitische. Sijui ni serikali, sijui nini; haya ni mambo ya kupotoshana. Swala muhimu ni kwamba hii irudiwe ikakaliwe kwa umakini na wale ambao walikuwa wavivu katika zile Kamati zao wabadilishwe wawekwe katika Kamati nyingine kwa sababu maswala ya Afya kama vile mheshimiwa Peter Ziro alivyozungumza ya kwamba inaoana na maswala ya maji.

Kwa mfano, swala la afya sio swala la kuchezea. Swala la afya ni maisha ya mtu na ikiwa ni maisha ya mtu ni lazima tuipatie kipaumbele. Hapa ndani ya Bunge saa hizi tukianza kuulizana ni Kamati gani imefanya kazi, mheshimiwa Spika nakuhakikishia ya kwamba Kamati ya Bajeti itasifiwa, Kamati ya Elimu itasifiwa ikichanganywa na zile za *Scholarship*. Kuna nyingine hazitasifiwa kwa sababu utendakazi wao uko chini. Ingekuwa ni kupeanwa *marks* na kupeanwa vithibitisho na Ripoti zinavyokwenda, Kamati ya Afya ingekuwa ndio zero kabisa na ndio maana nasema...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Thaura, if you want to say something please rise up. If you want to rise on a Point of Order we have the intervention button.

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, nafikiri hapa juu tunapata matatizo kidogo kwa sababu inakua vigumu kusema ni *Point of Order* ama tunataka kuchangia kwa sababu najua wao...

The Speaker (Hon. Kahindi): Let us operate like this. If you have a Point of Order, just stand up and shout Point of Order...

Hon. Thaura: Na kama unataka kuchangia? Kwa sababu...

The Speaker (Hon. Kahindi): Stand up as well and say that...

Hon. Thaura: Nilikua nahitaji kuchangia.

(Hon. Mwayaa stood on a Point of Order)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay fine, I will write your name down. Yes, hon. Mwayaa, you have a Point of Order?

Hon. Mwayaa: Asante Mheshimiwa Spika. Nilikuwa nimesikia Mheshimiwa Ndago akisema kwamba kuna waheshimiwa wengine ni wavivu na waondolewe kutoka kamati hii hadi kamati nyengine na nikaona anapotosha hili Bunge kwa sababu ni kama ambaye hiyo Kamati ambayo atapekwa huyo *Member* ambaye ni mvivu hatafanya kazi na Bunge hili tunataka tufanye kazi. Alikuwa anafanya haki akisema hivyo ama anapotosha hili Bunge na wote walichaguliwa katika Bunge hili?

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Ndago.

Hon. Ndago: Mheshimiwa Spika, nataka kumfahamisha mheshimiwa Mwayaa kwamba saa nyengine wakati unapika chakula unachagua; kwa mfano, unapika mahindi na maharagwe unachagua. Kuna tembe ambazo zinakufaa na zingine hazikufai. Ikiwa unaona leo siwezi kula maharagwe peke yake unaweza kuchanganya mahindi na maharagwe ikawa *githeri*.

Kwa hivyo, wale ambao hawawezi kufanya kazi kule kama Mwenyekiti aletwe huku awe mwanakamati. Ndio maana nasema akija huku akiwa Mwanakamati ataona yule mwenzake anafanya kazi kisawasawa.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha ikiwa Kamati hizi zitapitishwa kwa kuwa ni maswala ya serikali. Mimi sipingi serikali lakini ikiwa ni swala tu la kuwa tupitishwe kwa kuwa ni Mswada wa serikali nataka nimuambie ndugu yangu mheshimiwa Dickson Shaban ya kwamba serikali wakati mwengine inakula watu wake. Utatafunwa! Usikubali kupakwa mafuta kwa mgongo wa chupa. Asante.

Hon. Kenga: Mheshimiwa Spika, rafiki yangu na jirani yangu mheshimiwa Ndago ni maneno mazito anayotamka kulingana na utendakazi wa Kamati ya Afya. Nilidhani Mwenyekiti wa Kamati aliposimama alikuwa na nia ya kujitetea lakini akasema kwamba atachangia baadaye kama ulivyomuelekeza. Nasema hivyo kwa sababu nimeangalia wanakamati wa Afya mbali na wale wengine ambao walijalizwa wakati kulipofanywa marekebisho na Kamati husika na wa kwanza kabisa ambaye ni Mwenyekiti ni mheshimiwa Thaura Mweni, wa pili ni mheshimiwa Mary Anzazi Maneno na wa tatu ni mheshimiwa Martha Koki Musyoki, Edward Kazungu Dele, Albert Kiraga ambaye kwa sauti nimesikia kwamba yeye ni daktari ndani ya Bunge hili, Caroline Kalume, Thomas Mumba Chengo, Alphonse Mwayaa ambaye ni *Majority Whip*, na Sabrina Tumaini. Mimi nataka niamini kwamba hiki kikosi ni kikosi cha nguvu na kazi bila shaka wanaifanya nikiamini kwamba wakati fulani tulimuita Waziri wa Afya mbele ya Kamati hii na kuhojiwa kwa maswala fulani ambayo yalikuwa yamefanyika. Labda tu sijui ni kwa misingi gani pengine itaonekana hawa ni walegevu lakini kama ni walegevu nafikiri wana haki ya kuji...

(Hon. Chiriba stood on a Point of Information)

Hon. Chiriba: I want to inform the current Member on the Floor...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kenga, do you to be informed?

Hon. Kenga: Ni Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Elimu na tunafanya kazi kwa ushirikiano na nadhani anayoyazungumza ni kwa ajili ya kunijenga.

Hon. Chiriba: Asante. Nilikuwa nataka tu niweke mwanga kwa wakati aliposema kwamba ni kikosi cha nguvu. Nataka kumjulisha kwamba nguvu hazidhihirishwi na ile misuli ambayo tungeiona kwa mtu; zinadhihirishwa na utendaji kazi. Kwa hivyo, mheshimiwa Ndago naona bado yuko kwa njia ya sawa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Kenga: Asante kwa ufahamu huo lakini nilikuwa sijakamilisha. Naomba sasa nikamilishe. Amepeana mifano ya baadhi ya Kamati ambazo zimeonekana zikifanya kazi kwa hali ya umakini na moja ya ile mifano ile imepeanwa ni Kamati ya Bajeti ambayo Mwenyekiti wa Bajeti pia ni mwanakamati katika Kamati hii lakini sasa swala ambalo linajotokeza ni katika hali ya kuelewa kwamba saa hii tunaenda kwa rekodi; tunasema kwamba Kamati ya Afya ni legevu ndani ya Bunge letu. Labda hapo mheshimiwa Spika utufafanulie.

Hon. Ndago: Mheshimiwa Spika, nafikiri mheshimiwa Naibu wa Spika akiwa atasimama na kuunga mkono huo ni uamuzi wake. Amesoma hayo majina vizuri na akawapongeza lakini nataka nikumbuke ndani ya Bunge hili kwamba mheshimiwa Stanley (Kenga) alikuja akalalamika na akalia kuhusu zahanati ya Adu kwamba utendajikazi wa Kamati haukuwa mzuri na hata alipojibiwa Ripoti yake pia haikumfurahisha. Sasa leo hii amesimama kidete anasema hawa ni wachapa kazi. Mimi hili si swala la kwamba tuwe tutalichukulia kwa wepesi. Ni swala la kuchukuliwa kwa uzito na umakini. Vile anavyozungumza mimi nimemuamini kwamba semi zake huwa za umakini.

(Hon. Thaura stood on a Point of Order)

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, ndugu yangu ambaye ni Naibu katika upande wetu wa walio wengi Bungeni mheshimiwa Ndago nafikiri amepotoka kwa kutoa taarifa ambazo sio sahihi. Tutakubaliana kwamba kipindi sio kirefu tulikuja tukakagua katika uteuzi wa kumpatia mmoja wetu ambaye alikuwa anachukua kazi ya Katibu mtendakazi katika Kaunti yetu ya Kilifi. Mheshimiwa Ndago ni mmoja katika wale waheshimiwa ambao hawana misimamo na hiyo siku nilikuwa nimeketi kiti ambacho kiko kati ya mheshimiwa Mchungaji na mheshimiwa kiongozi wa walio wachache Bungeni na siku hiyo nilisema itakuja siku ambapo tutakumbuka yale maneno mazito ambayo nilikuwa nayazungumza pale na ni kwa sababu sisi Kamati tulikuwa na mda wa kuangalia tajriba ya yule bwana na tukaona kwamba kulikuwa kuna ati ati katika tajriba yake.

Tunavyozungumza jana hapa tulikuwa na waziri na timu yake na tulizungumza faraghani lakini acha niwaambie kwamba ipo kasoro kubwa katika kile kitu ambacho mlikifanya ile siku na hatujasahau kwamba kuna wengine walipata kitu kidogo katika sehemu ambazo sio sahihi za mtu kama mheshimiwa kufanya kitu kama hicho.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Thaura, you know you stood up on a Point of Order. I want you to address yourself on the Point of Order.

(Hon. Ndago stood on a Point of Order)

Hon. Ndago: Mr. Speaker, I just want to get a clarification whether the Committee brought one Report or they brought two? I am aware that the first Report was supposed to be the first Report but later on the Chairman misled the Committee that is why he is crying that some of us, me included were not straight forward. I want to inform him that this is politics and he is in the House of politics and he must be smart or people will outsmart him.

He is the one who led the Committee in making the Report. Infact he is the one who is not straightforward; he brought two Reports. Today we are not discussing the Report that was brought by the Committee. We are discussing about the Report on approval of the Selection Committee that was brought before this House.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, I think I am not misleading the House if I quote what the hon. Member has just said. I am just giving information on what is supposed to be done not unless he is the one misleading the House yet he is the Chair of that Committee. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Let me clarify on something so that we don't have so many Points of Order. Let us be guided by what is before us so that we give room to people who want to contribute to the Motion. We have hon. Kiraga. Hon. Chengo (Mumba) do you want to contribute or is it a Point of Order? Your button is on the intervention.

Hon. Mumba: It is a Point of Order and I want to make something very straight here because I have been mentioned as a Member of the Committee on Health so I want to clear my name on...

The Speaker (Hon. Kahindi): You have been mentioned by virtue of being a Member...

Hon. Mumba: Yes, that is why I am standing on a Point of Order as per the Standing Orders that are here.

The Speaker (Hon. Kahindi): You are raising a Point of Order to whom?

Hon. Mumba: The Member who was on the Floor. I dialed this thing a long time ago; it is only now that I have dialed the intervention button.

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Kahindi): No I did not see it. I am sorry. So now you want to make a Point of Information to whom?

Hon. Mumba: It is not a Point of Information because I know you will deny it. It is a Point of Order.

The Speaker (Hon. Kahindi): It is procedure...

Hon. Mumba: It was there before you ruled on the Point of Orders. My button was already on unless you want to deny me this opportunity but there is very important information I want to pass across here.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, what is your Point of Order?

Hon. Mumba: Mr. Speaker, I am a very keen listener and a man of few words and I always watch what I say after what I have gathered. With all due respect, if I might quote the Standing Orders on the contents of speeches, I think it is a direction that we should be guided under Standing Order No. 83(4), if you allow me to read;

“No Member shall impute improper motive to any other Member except upon a specific substantive Motion of which at least three days' notice has been given, calling in question the conduct of that Member or Senator’.

It is very unwise if you can rise and say that a certain Committee is not working while you cannot substantiate whatever you are saying. So, being a Member of that Committee I feel insulted. I feel that at least to a point; my dignity has been damaged because I believe I offer my best when it comes to Committee work.

So being a Member of that Committee to generalize that the Committee Members are not working I think as per this Standing Orders, I feel that my dignity is ruined. I believe I always offer my best when it comes to Committee work. I thought it was very wise now to make it clear that whenever we are pointing out any allegations they might be correct or wrong but let them be

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

directed to the right Member of a Committee or whoever deserves that information. That is the information that I wanted to pass across, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. For that same reason is why I ended the debate on hon. Ndago and hon. Thaura. For any avoidance of doubt, if you have pressed the button and I am not responding just raise your hand because I did not see your intervention here. Hon. Kiraga, yes proceed.

Hon. Kiraga: Thank you Mr. Speaker. First of all, I want to say I am against this Motion. If the law has to be followed then it should be followed wholly, not partially. If you go the County Governments Act Section 14 (1), the Committee has obeyed that Section but when you come to the Standing Order No. 161, the Committee obeyed some Sections and left out some of them. Standing Order No. 161 (1) (a), the Membership of each Committee reflects the relative majorities of the seats held by each of the Assembly parties or coalition of parties in the county Assembly, that has been obeyed. But if you go to (b), no two Members of the House Business Committee serve in the same Sectoral Committee. That section alone has compelled me to go against this Report.

I want to give examples of this list. If you go to Water, Environment and Natural Resources, can we confirm that hon. Valentine Matsaki sits in the HBC (House Business Committee)? Can we also confirm that hon. Alphonse Mwayaa sits in the HBC? Hon. Sabrina Tumaini sits in the HBC too. That is one Committee; there are several Committees that have not obeyed the Standing Orders.

The Speaker (Hon. Kahindi): Can we confirm that because you are raising a very pertinent issue. Hon. Matsaki, are you a Member of the HBC? Hon. Mwayaa, are you also a Member of the HBC? Hon. Sabrina Tumaini, are you a Member of the HBC?

Hon. (Ms.) Tumaini: No!

Hon. Kiraga: Although she's not a Member but what does this note say? Not two Members, that means only one Member. If you go to the other lists, you will also find more than three Members. Let us go to Trade, Tourism and cooperatives; we have hon. Peter Ziro...

The Speaker (Hon. Kahindi): Ho. Peter Ziro, are you a Member of the HBC?

Hon. Ziro: Yes.

Hon. Kiraga: We have hon. Christopher Mwambire.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Christopher Mwambire, are you a Member of the HBC?

Hon. Mwambire: Yes.

Hon. Kiraga: Yes, these are two Members sitting in the same Committee. These Standing Orders say no two Members of the HBC serve in the same Sectoral Committees.

(Loud consultations)

So hon. Speaker, let us get the Members of the HBC we countercheck with this list. The Standing Orders must be obeyed.

Hon. Mbura: Asante Bw. Spika. Nasimama kupinga Ripoti hii. Kwanza kuna Kamati ya *Delegated County Legislation*; hii ilikuja kama Hoja ya mwanzo kabla ya mabadiliko ya hizi Kamati nyengine na iliregeshwa kwa ajili mheshimiwa Emmanuel Changawa alikuwa katika hii orodha. Iliporudi, marekebisho zaidi yalikuwa yametendeka kwa mfano jina langu lilikuwa katika hii Kamati lakini ilirudi ikiwa jina langu haliko na tuliiregesha kwa ajili ya marekebisho ya Emmanuel Changawa lakini nimeona kuwa Ronald Mbura ndiye aliyeenda akatolewa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Lengine ni juu ya kuunga mkono mheshimiwa mwenzangu Peter Ziro wa Garashi. Amezungumza jambo muhimu sana juu ya Kamati ya Maji kwamba kwa vile ni Kamati muhimu hasa kwa afya yetu, ingekuwa vizuri kila *Sub-County* iweze kupata mwakilishi.

Hali hii hii inanikumbusha nyakati za nyuma na hali hii ndio imefanya Kilifi South haipati wawakilishi wa kutosha katika Kamati ya Bajeti maanake tunaona waheshimiwa hawaonekani katika vikao ilhali tulisimama tukasema kwa nini huyu ndiye aliyeungwa mkono lakini najua ni siasa iliyoweza kugeuza matakwa yetu. Lakini hali hii ndio inaathiri Kilifi *South* maanake mheshimiwa mmoja kutoka Kilifi *South* ambaye anatuwakilisha sisi katika Bajeti katika vikao na ikiwa anaonekana lakini si wakati ule muhimu wa kujadili na kututetea sehemu ya Bajeti katika Kilifi *South*. Kwa hivyo ninaomba ...

(Hon. Mwathethe stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Mwathethe, you have a Point of Order?

Hon. Mwathethe: Bwana Spika, nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii sitaki kutetea hii Ripoti bali nataka waheshimiwa wawe huru kutoa maoni yao lakini jinsi wanavyotoa malalamishi pia nataka nipate mafundisho na maelekezo. Mtu akisema Kamati ya Maji ni Kamati muhimu sana ningetaka pia niambiwe zile ambazo si muhimu sana ni zipi? Ndio wakati tunakaa sasa kulingana na ufahamu ambao nitakuwa nimepata hapa nijue hii ni muhimu naweza weka huyu na hii si muhimu naweza weka huyu. Kwa hivyo mheshimiwa anielezee, Kamati ya Maji imetajwa hapa mara mbili kwamba ni muhimu, zile ambazo si muhimu hapa ni zipi? Ambazo tunaweza weka tu ...

The Speaker (Hon. Kahindi): And who is supposed to sit in which one...

Hon. Mwathethe: Naam, anielezee na ni nani na nani awekwe wapi. Tunajua wengine ni walegevu sasa wawe walegevu tuwapeleke wapi? Mheshimiwa Spika, ili kwamba wakati tutakapokaa tena tuwe na ufahamu mkubwa na mzito wa kujua mlegevu ni fulani na anatakiwa kwenda katika Kamati fulani ndio tusiende kukaa na tukarudi. Mambo kama hayo mheshimiwa Spika. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, hon. Mbura, you have heard the Leader of Majority. He wants to know which are these Committees that are not important? Kindly press your microphone.

Hon. Mbura: Asante Bwana Spika. Kusema kweli, haimaanishi kwamba Kamati nyengine si muhimu lakini kwa shughuli zinazohusika lazima tutaziweka kwa kundi ambalo ni muhimu zaidi ya nyengine. Ninasema hivyo kwa sababu, kwa mfano Kamati ya Bajeti. Kamati zote hizi zinaangazia hasa Kamati ya Bajeti kwa *resource allocation*. Hii naiona pia ni muhimu kushinda nyengine kwa sababu bila hii, zile Kamati nyengine pia utendakazi wake utakuwa mgumu. Kwa hivyo tunapozungumzia Kamati ya Maji pia tunasema hivyo kwa sababu ina *cut across* Kamati nyingi ambazo...

(Hon. Kadenge stood on Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kadenge, you have a Point of Order?

Hon. Kadenge: Mheshimiwa Spika, nataka utupatie mwelekeo. Kulingana na ile Standing Order ambayo mheshimiwa wa Gongoni ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bajeti ametupa ameingea vizuri sana lakini bado wewe hujatupatia mwelekeo kama...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): He has not requested me to do anything; he made his contribution in relation to that Standing Order.

Hon. Kadenge: Lakini imefuatwa hiyo sheria?

The Speaker (Hon. Kahindi): I don't know. If he requested me to do anything, I would do so by a way of a Motion.

Hon. Kadenge: That is why we need your guidance also...

The Speaker (Hon. Kahindi): My guidance is, make contributions then I will ask if you have anything else.

Hon. Kadenge: I think we need a way forward from the Chairperson.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kadenge, hon. Kiraga has noticed something; if he wants to proceed there is a way to proceed under the Standing Orders otherwise to me that is his contribution.

Hon. Kadenge: Okay, nikiileta hivi kuwa utupatie mwelekeo kulingana na hii *Standing Order* utatuambia nini Spika?

The Speaker (Hon. Kahindi): The Standing Order says "no two Members"...

(The hon. Speaker spoke off record)

Hon. Kadenge: Hapana, si hiyo *Standing Order* inasema "no two members" ndio hiyo twataka kujua kama imefuatwa maanake ukiangalia haikufuatwa.

The Speaker (Hon. Kahindi): Then that should be deliberated in a different way; you cannot say I give direction on things that have not been requested to give direction.

Hon. Kadenge: Okay, hiyo haikufanyika, wewe unatupatia mwelekeo gani?

The Speaker (Hon. Kahindi): What does the Standing Order say?

Hon. Kadenge: "No two Members"...

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, Meaning?

Hon. Kadenge: Ya kuwa isiwe zaidi ya mtu mmoja...

The Speaker (Hon. Kahindi): How many Members are there?

Hon. Kadenge: Wawili wawili...

The Speaker (Hon. Kahindi): So, I put that question as deliberation. It is upon you now to decide. That is why there is a question at the end of the debate. Because you see if a ruling is passed out of this that is a separate thing...

(The hon. Speaker spoke off record)

Now, the issue is whether two Members or more have been put in each and every Committee. The issue is what has the House resolved? That is why I put the question at the end of the debate. However your question is you cannot have two Members from the House business Committee.

Hon. Kadenge: Exactly.

The Speaker (Hon. Kahindi): Now that is what you...

(The hon. Speaker spoke off record)

... and I have heard people saying more; there is no word more unless we have different Standing Orders. 'No two' means you cannot have two, but you see I cannot take your seat.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Kadenge: Mheshimiwa Spika pole, pole lakini ikiwa tuna *discuss* orodha ambayo haikufata sheria za *Standing Order* zetu kuna umuhimu kweli kuendelea na hii?

The Speaker (Hon. Kahindi): It doesn't mean that the debate has to be removed.

Hon. Kadenge: Okay, thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, let me just explain. When I sit here, I am not supposed to change what is what is in the debate. You are supposed to see things and then you move. Last time there was an issue. I am a referee you cannot tell me pass the ball to number nine to score; so, you grab it. However, that does not mean more because the word 'more' is on the list, it simply means 'no two' the same way it was said 'no three Members'; if you have three Members that means you have gone wrong. Are we together, hon. Kadenge?

Hon. Kadenge: Yeah, it is okay.

The Speaker Hon. Kahindi: Yeah...Hon. Deputy Speaker (Kenga) you have a Point of Order?

Hon. Kenga: Contribution.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay... Hon. Mbura Proceed. Hon. Mwayaa, you have a Point of Order?

Hon. Mwayaa: Yes.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, hon. Mbura take your seat.

Hon. Mwayaa: Mheshimiwa Spika, hii ni Nyumba ya siasa ndiyo lakini naona kidogo mheshimiwa Mbura ni kama amekosa mwelekeo wakati amesema kwamba anaunga mkono mheshimiwa wa Garashi ambaye amesema kwamba Magarini hakuna mwakilishi upande wa maji. Kisha yeye akarudi tena mheshimiwa Mbura akasema yeye yuko na mwakilishi ambaye hawajibiki upande wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa ukiangalia hapo kidogo kuna mvutano ambao ...

The Speaker (Hon. Kahindi): Let me make something very clear. When it comes to Membership of Committees it is not about regions unless you change the Standing Orders like we did in the last term where we included that Members of the Budget Committee should come from each and every Sub-County. However, it is a political party issue. So if you continue with the argument based on where you come from it is misleading. I did not want to say that but you see now, I am not supposed to but you are supposed to know. You are supposed to read the Standing Orders and know that you cannot stand here and argue that this Sub-County does not have people. In the year 2013/2017 we amended the Standing Orders and we included that in the Budget Committee, Membership shall be derived from each Sub-County.

At that particular time one would stand up and say there is no representation from Magarini because the Standing Orders say that Membership of this Committee must be derived from each and every Sub-County. In this case, I know you are trying to persuade your Members but you know it proves your ignorance when you say that we do not have representation from this Sub-County whereas under Standing Order No. 161 it is very clear; membership is on the strength of parties. So that is why the Leader of Majority is getting concerned because your line of argument does not help him to do a better job.

Can you kindly make your contributions based on the Standing Orders and when the standing Orders say 'no two' it means you cannot have two and if you have it is not my business to tell you what to do, you are supposed to know; that is why you are here. The issue is, if that makes it defective the question comes to you, would you say *Aye* or would you say *Nay* or alternatively you can still move a Motion and say let these people go back because they have not complied. You know I do not want to turn this into a lecture room but I presume you should

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

know these things. Are we together hon. Members? So, your continued argument that my area is not represented that is a fallacy because the law on membership to parties is not about where you come from, it is not about where there is no water, it is not about where there is no electricity, it is about which party and the strength of the parties. Now I think we are clear on that. I will still give you a minute hon. Mbura to finish.

